HOTUBA YA MHE. MAMA SALMA KIKWETE WAKATI WA KUZUNGUMZA NA WANAWAKE WA WILAYA YA ILALA, TAREHE 28 APRILI, 2010

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ndugu William Lukuvi

Mhe. MNEC wa Mkoa Wa Dar es Salaam, Ramadhan Madabida

Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Ndugu Selemani Karanje,

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Dar es Salaam,

Bibi Zarina Madabida

Mwenyekiti wa UWT (W) , ILALA , Bibi Aaliha Riyami,

Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dar es Salaam, Bibi Janet Masaburi

Mjumbe wa Baraza Kuu la U.W.T. (T) Angela Kairuki

Waheshimiwa Madiwani wote Mliopo Hapa

Viongozi wote wa Chama na Serikali,

Ndugu Akina Mama, Wageni waalikwa

Habari za Leo!

Naomba mniruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuwepo hapa siku ya leo. Aidha, nichukue fursa hii kuwapongeza viongozi wote na akina mama kwa ujumla kwa kuweza kufanikisha shughuli hii. Nimefurahi sana kupata fursa hii ya kuweza kukutana na wakinamama wengi ambao kwa dhati kabisa wameweza kuonyesha juhudi zao katika kujikwamua kiuchumi.

Pia nichukue fursa hii kuwafikishieni ujumbe kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Ndg. Jakaya Mrisho Kikwete, anawasalimu sana!

Ndugu Viongozi, Mabibi na Mabwana

Leo tumejionea shughuli mbalimbali za wanawake ambazo zinaashiria kuwa wanajituma kwa jitihada kubwa ili kujiletea maendeleo.

Hongereni sana! Hata hivyo sote tumesikia changamoto mbalimbali ambazo zinawakabili. Baadhi ya changamoto hizi zimo ndani ya uwezo wa Halmashauri hii ya Ilala.

Nina imani kuwa Wilaya ina idara inayoratibu shughuli hizi za wanawake ili kuhakikisha wanawake wanapata huduma zinazostahili na kwa utaratibu uliopangwa na serikali. Hivyo tusimamie taratibu hizo vyema ili kutatua changamoto zilizopo. Lakini pia, wanawake wengi hushiriki katika kufanya biashara ndogo ndogo. Ni wajibu wetu kuwasaidia waweze kuondokana na biashara ndogo ndogo ambazo zina faida ndogo ambayo mara nyingi hutumika kwa kujikimu katika mahitaji ya familia, badala ya kuwaletea maendeleo. Lengo la kumsaidia mwanamke ni kumtoa katika hali aliyonayo sasa na kumfikisha mahali ambapo atakuwa na maisha bora zaidi.

Ndugu wananchi

Leo tuko hapa kwa ajili ya kuzungumza mambo ya Maendeleo. Wanawake lazima tutambue kuwa ili tuweze kufanikiwa katika hili lazima tushirikiane kwa dhati. Tuungane mkono pale inapobidi kufanya hivyo, tuelekezane, tuelimishane, na tupeane moyo. Haya yote yatawezekana ikiwa tutakuwa na upendo ambao utajenga urafiki baina yetu. Kwani kauli mbiu ya ULINGO inasema, ***"Rafiki wa Mwanamke ni Mwanamke"!***.. Kwa kufanya hivyo tutajiondolea vikwazo na chuki baina yetu. Tuache kufuata misemo kuwa wanawake hatupendani! Hayo yamepitwa na wakati!. Tubadilike na kuanzia sasa tukubaliane kuwa ***"Rafiki wa Mwanamke ni Mwanamke bila kujali itikadi zetu!".***

Ndugu Wananchi

Wanawake tunakabiliwa na matatizo mbali mbali katika maisha ya kila siku. Matatizo hayo ni pamoja yale yaliyo katika elimu, afya, na mengine mengi ya kijamii. Mimi binafsi, kwa kutambua matatizo ya mwanamke, niliamua kuanzisha taasisi ya Wanawake na Maendeleo kwa kifupi WAMA. Ili niweze kutoa mchango wangu wa kuwasaidia wanawake wenzangu. Katika kutekeleza azma hii taasisi ya WAMA imeunda vitengo vinne ambavyo ni ***Elimu ya mtoto wa kike, Afya ya mama na mtoto, Watoto yatima,*** *na* ***Uwezeshaji wanawake.***

Ndugu wananchi

Pamoja na matatizo yanayotukabili wanawake, bado wanawake tuna jukumu kubwa katika jamii yetu. Katika hili napenda kuzungumzia suala la ***malezi.***

Kwani mwanamke ndiye mlezi wa familia, hivyo ana mchango mkubwa katika kuelekeza maadili mema katika ngazi ya familia na hatimaye Taifa kwa ujumla. Hivyo ni wajibu wetu kuwaelekeza watoto wetu malezi yaliyo mema ili kuepuka mmomonyoko wa maadili.

Vijana wetu wa sasa, wametekwa na mambo ya utandawazi. Si vibaya kuwa katika ulimwengu huu wa utandawazi, bali lazima tuwaase vijana wetu wachague mambo ya kuiga. Ni vizuri wakaiga mambo ya maendeleo na teknolojia, lakini mila na desturi za nchi nyingine zisituharibie ustaarabu wetu. Wilaya ya Ilala ni miongoni mwa Wilaya tatu za Mkoa huu wa Dar es salaam, ambayo ina watu wengi sana ukilinganisha na ukubwa wa Mkoa huu.

Na kila mmoja wetu anafahamu kuwa jiji hili lina mambo mengi yanayofanyika kinyume na maadili na kupelekea kuwa na vijana wasio waadilifu.

Wazazi na walezi, tusikwepe majukumu kwa visingizio mbalimbali kama vile ugumu wa maisha. Tushirikiane katika malezi na kupambana na tabia mbaya zinazoharibu vijana wetu.

Ndugu wananchi

Jambo lingine ni kuhusu suala la ***UKIMWI***. Hili lazima tulizungumze wazi wazi ili kupunguza kasi ya maambukizi. Kwani tusipolizungumzia suala hili, tutapoteza nguvu kazi, yaani vijana ambao ndio nguzo ya Taifa letu. Ni vyema tukaongeza jitihada za kupambana na suala hili ikiwa ni pamoja na kukemea tabia hatarishi. Kwani Mkoa huu ni miongoni mwa mikoa ambayo ina kiwango cha juu cha maambukizi.

Nashauri sisi tuliopo hapa tuwe mfano kwa kupima afya zetu, kuacha tabia hatarishi na kuelimisha jamii inayotuzunguuka.

Nina imani kabisa tutakuwa tumetoa mchango mkubwa katika kupunguza kasi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Wakina mama muwashawishi wakina baba kwenda kupima afya na kuchukua hatua zinazostahili.

Ndugu Viongozi, Mabibi na Mabwana

Mwisho kabisa naomba nimalizie kwa kuwakumbusha kuwa, Mwaka huu ni Mwaka wa uchaguzi. Hivyo kila mmoja wetu ana wajibu wa kutambua kiongozi anaemfaa. Tusipoteze muelekeo kwa vishawishi na maneno ya kukatisha tamaa kwani sote tunafahamu kuwa *kuleta Maendeleo ya nchi sio kazi ya usiku mmoja!* Hivyo tuchambue mambo na tufanya maamuzi sahihi!.

Baada ya kusema hayo niwashukuru na kuwatakia kila la kheri .

Mungu wabariki wakina mama, Mungu ibariki Tanzania.

Ahsanteni Sana kwa kunisikiliza!